Kumb: FemAct/Barua/01 Tarehe 22 Octoba 2001

BARUA YA PONGEZI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MH. BENJAMIN MKAPA

Mheshimiwa Rais,

Sisi wanaharakati wa masuala ya Jinsia, Haki za Binadamu na Maendeleo tunapenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa ujasiri mkubwa ulioonyesha katika hotuba yako ya tarehe 30 Septemba mwaka huu. Mara kwa mara tumekuwa tukifuatilia kwa makini hotuba zako unazozitoa kila mwisho wa mwezi. Hotuba yako ya mwezi Septemba, 2001 ilionyesha kwa taifa ujasiri mkubwa na uchungu ulionao kuhusu nafasi waliyowekwa wananchi wako katika suala zima la uchumi wa ulimwengu.

Tunafurahi kufahamu kuwa bila shaka wewe mheshimiwa Rais, pamoja na serikali yako mnauelewa mtazamo wetu kuhusu mfumo wa uchumi wa dunia na jinsi unavyoathiri uwezo wa nchi zinazoendelea na maisha ya raia wa nchi hizo hasa wale wa nasaba za chini. Haya ndiyo masuala ambayo sisi wanaharakati tumekuwa tukiyapigania na kuyatetea siku zote. Tumefarijika sana kuona kuwa masuala haya ndiyo yaliyokuwa kiini cha hotuba yako hiyo ya mwezi Septemba.

Tukiangalia kwa upana suala la mahusiano ya kiuchumi yasiyo sawa kati ya nchi tajiri na maskini utaona jinsi linavyofungamana na sera za urekebishaji wa uchumi, ambapo nchi inalazimishwa kufuata masharti ambayo yanawaumiza sana wananchi hususani wanawake, watu wenye ulemavu, vijana wa kike na wakiume pamoja na wanaume maskini. Baadhi ya masharti hayo ni kama vile kupunguza wafanyakazi ambao mara nyingi wanaoathirika ni wale wa kipato cha chini na kupelekea maisha yao kuwa duni kupindukia. Sanjari na hilo tafiti zinaonyesha kuwa ukosefu wa ajira umewafanya vijana wengi tena ambao wanasomeshwa kwa kodi za wakulima na wafanyakazi maskini wa Tanzania kuwa mzigo mkubwa kwa familia na taifa hili. Si hivyo tu, kuondolewa kwa ruzuku katika pembejeo za kilimo na kujiondoa kwa serikali katika usimamizi wa soko, kumekuwa ni kero na taathira zake zimekuwa mbaya sana kwa uwezo wa kujikimu kwa jamii nyingi za wakulima na wafugaji wadogo. Ukichukulia kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu, haiyumkini kuwa shinikizo hili la mashirika ya fedha ya kimataifa lilikuwa na nia ya kuvunja kabisa kitovu cha maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Rais,
Iko mifano ya kutosha kuonesha jinsi ambavyo mabadiliko ya sera za uchumi baada ya shinikizo la mashirika haya yanavyowaathiri wakulima na wafugaji wadogo, hasa kwa kuwa hakuna miundombinu ambayo wanaisimamia na

kuwa na sauti nayo inayoweza kuwawezesha kupata pembejeo kwa bei nzuri na ikiwezekana kwa mikopo, kupata taarifa kuhusu hali ya soko la kiulimwengu na

kufikisha mazao yao sokoni. Kwa hali hiyo, wafanyabiashara binafsi ambao wanazingatia faida za haraka zaidi ya jambo lingine lolote lile, wametumia mwanya huu kuvunja kabisa nguvu ya wananchi, wanawake kwa wanaume, kuwekeza kupata mapato ya haki kwa mazao yao ya kilimo. Jambo hili lina athari za muda mrefu kwa uchumi wa taifa letu.

Mara nyingi uwekezaji umekuwa haufanyiki katika misingi ya kumwendeleza mwananchi na badala yake unakuwa ni ujanja wa kuhamisha mali na rasilimali za taifa. Kwa mfano, kwenye sekta ya madini, wakati wachimbaji wadogo wadogo walikuwa wanalipatia taifa hili pato kubwa kutokana na kuuza madini katika benki yetu, wawekezaji wakubwa walioingia wamewatoa wananchi hao katika ajira hiyo. Hatujui kwa nini mfumo wa ununuzi wa madini kwa kutumia mabenki ulifutwa.
Taarifa za watafiti zinaonyesha kuwa tangu mfumo huo ukome na wachimbaji wakubwa kuingia, kiwango cha uzalishaji wa madini, kwa mfano Tanzanite ambayo hupatikana hapa nchini tu, kimeongezeka mara dufu lakini rekodi za ulipaji wa kodi hazionyeshi ongezeko hilo. Hii inaonyesha wazi kuwa rasilimali hiyo inahamishwa kwa wingi kiujanja.

Pamoja na kwamba vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti juu ya hali hiyo na wananchi mbambali kulalamikia baadhi ya wawekezaji wanaohamisha hata udongo kwa visingizio kwamba hakuna mashine za kupima madini hapa nchini, hatuoni hatua zozote zikichukuliwa kurekebisha hali hiyo. Ukweli ni kwamba jambo la kuhamisha udongo makontena kwa makontena linawapa wananchi wasiwasi kuhusu sababu hasa ya kitendo hicho. Mheshimiwa Rais, mazingira yanayopelekea mambo haya kufanyika yanaashiria kuwa rushwa inatumika.

Mheshimiwa Rais, kwa maoni yetu,wawekezaji wangewekeza katika viwanda vyetu vya nguo, viatu, usindikaji wa vyakula, mazao, na hata vya kutengeneza vito vinavyotokana na madini na njia za usafirishaji ili na sisi tuweze kuwa na uwezo wa kuingia katika nafasi nzuri ya ushindani. Kipindi cha kuuza mali ghafi nje badala ya kuisindika na kuiuza sokoni tayari kwa mlaji kimepita na tukiendelea na mfumo huo hatutaondokana na nafasi tuliyowekwa wakati wa ukoloni ya kuwa vyanzo vya malighafi kwa ajili ya viwanda vya nje.

Vilevile, mfumo wa uzalishaji wetu wa kuzalisha tusichotumia na kula tusichozalisha unatuweka katika hali mbaya ya kutojijengea mazingira na kuwa na uhakika wa chakula na uchumi himilivu. Sisi tunaona kuwa wawekezaji wa nje wenye dhima ya kuendeleza nchi hii kiuchumi ili kupambana na umaskini hawapo. Katika mfumo wa utandawazi wa kibiashara kama ulivyokiri wewe mwenyewe mheshimiwa Rais, sisi tunasema kuwa mataifa tajiri kutupangia bei za mazao yetu ni unyanyasaji na udhalilishaji wa wazalishaji maskini wa nchi hii; wanawake, watu wenye ulemavu, vijana wa kike na wa kiume pamoja na wanaume maskini. Isitoshe mheshimiwa Rais wakati wananchi wa mataifa tajiri wanapatiwa ruzuku katika uzalishaji hapa wanashinikiza kuziondoa katika maeneo yote!

Kwa upande wa mfumo wa kodi tunaona kwamba kodi nyingi zinawabana zaidi wanyonge, wanawake kwa wanaume, na kuwafanya kuendelea kukaa katika dimbwi kubwa la umaskini. Bila shaka serikali inahitaji kupanua wigo wa kodi ili iweze kutekeleza wajibu wake. Tatizo ni kuwa wawekezaji wakubwa wanapata mwanya mkubwa wa kukwepa kodi, na wazalishaji wadogo ndio wanaobanwa sana na mfumo wa kodi. Isitoshe, mfumo wa fedha unaelekea kutomjali kabisa mzalishaji na mfanyabiashara mdogo na wa kati, ambapo ndimo kundi kubwa la wazalendo walipo. Mabenki binafsi yana masharti ya mikopo na viwango vya riba ambavyo makundi

haya ya watu hasa vijana, wanawake na wanaume maskini hawawezi kabisa kayamudu, ilhali serikali imejitoa katika kujenga vyombo mbadala kama hatua madhubuti ya kuwawezesha wananchi kushiriki katika kuinua uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Rais, pamoja na hayo yote tuliyoyasema kumejitokeza minongóno ambayo hatuna uhakika nayo ingawa imeripotiwa kwenye vyombo vya habari kuhusu ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa serikali yako ambao kwetu sisi tuliamini kwamba watakusaidia katika vita dhidi ya umaskini na rushwa. Kwa mfano, shutuma zilizotolewa kuhusu matumizi makubwa ya fedha ya safari ya Waziri Mkuu katika nchi za Ulaya na Amerika yamezua minong'ono na manungúniko miongoni mwa wananchi ambapo yasipofuatiliwa na kufanyiwa kazi kwa ukamilifu yatapelekea wananchi wako kukosa imani na serikali yao. Wananchi wengi wanalalamika na kuhoji uhalali wa kutumia fedha nyingi kwa ajili ya safari za kuwahamasisha wawekezaji wa nje wakati fedha hizo zingeliweza kutumika kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi wa Tanzania ambao wamegubikwa na lindi la ufukara. Tunashauri kuwa wakati umefika kwa serikali yako na wewe mwenyewe binafsi kuchukua hatua za makusudi kabisa za kuwajengea wananchi uwezo wa kukabiliana na ufukara kwa kuwapa kipao mbele katika umilikaji na utumiaji wa rasilimali zipatikanazo hapa nchini.

Sisi wanaharakati tunamwona kiongozi anayefuja mali ya umma bila kuwa na huruma kwa wananchi wake kama mwekezaji anayehamisha utajiri wa nchi hii.

Mheshimiwa Rais, kwa ujumla wake, yale yote uliyoyataja ambayo sisi hapa tumesisitiza machache yake ni ya KUIFUKARISHA Tanzania na wananchi wake, wanawake, watu wenye ulemavu, vijana wa kike na wa kiume pamoja na wanaume maskini. Kamwe hatukubali kuwa Taifa letu ni maskini. Na kwa Ujasiri na Uhakika tunasema taifa hili ni tajiri na wananchi wake wanastahili kuwa na kauli juu ya utajiri huo.

Hivyo serikali yako ina jukumu na dhamana kubwa ya kulinda UTAJIRI huo ili usiendelee kuhamishwa kwa kisingizio cha uwekezaji. Kwa mantiki hiyo kuna kila sababu ya kurejea mikataba iliyowekwa kuhusu urekebishaji wa uchumi ili kulinda RASILIMALI za Tanzania na kuwanufaisha wafanyakazi na wakulima; wanawake, walemavu, vijana wa kike na wakiume na wanaume maskini.

Mwisho Mheshimiwa Rais, tumepata hamasa na kupewa matumaini kwani katika hotuba zako nyingi umekuwa ukimuenzi Baba wa Taifa na kusisitiza kuwa wajibu wetu watanzania ni kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo na kuendeleza yale aliyokuwa akiyapigania na kuyasimamia.

Na sisi tunaamini kabisa kuwa Mheshimiwa Rais una uchungu na nchi hii na kwamba uchungu huo hautaishia kwenye maneno tu bali utayatekeleza kwa uwezo na nguvu zako zote na sisi tunaahidi kuwa siku zote tutakuwa nawe bega kwa bega katika mapambano hayo.

Mungu Ibariki Tanzania.

Ni sisi:
1) Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)
2) Umoja wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (TANGO)
3) Taasisi ya Kitaifa ya majumuiya na Maendeleo ya Vijana (NYF)

4) Baraza la Habari Tanzania (MCT)
5) Chama cha Wanawake Wataalam (TWG)
6) Vijana wa Afrika (AY)
7) Changanyikeni Initiatives
8) Shirika la Kimataifa la Kutathmini Hali ya Kisiasa Afrika (PORIS)
9) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)
10)Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC)
11)Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA)
12)Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET)
13)Wakereketwa wa Juhudi za Maendeleo katika Afrika (ForDIA)
14)Tanzania Centre for Social Development (TACOSODE)
15)Maarifa ni Ufunguo
16)Mradi wa Utafiti na Uandishi wa Machapisho Juu ya Wanawake (WRDP)
17)Tanzania Traditional Energy Development and Environment Association (TATEDO)
18) Shirika la Mazingira Haki za Binadamu na Jinsia (Envirocare)

Imetayarishwa na Muungano wa Wanaharakati wa Jinsia, Haki za Binadamu na Maendeleo (FemAct).

Mh. Rais Benjamin William Mkapa,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P 9120,
Dar-es-Salaam.